**OFISI YA WAZIRI MKUU- TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA NAMTUMBO**

**NAMBA ZA SIMU:**

MKUU WA SHULE–**0762281200/0715281200**
MAKAMU MKUU WA SHULE–**0699189819**

SHULE YA SEKONDARI KORIDO

S.L.P.55
**NAMTUMBO**

…../……./2026

MZAZI/MLEZI WA…………
……………………..……….
S.L.P……………………………......……
……………………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KORIDO, HALMASHAURI YA WILAYA YA NAMTUMBO, MKOA WA RUVUMA.**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha tano katika Shule ya Sekondari **KORIDO** katika Tahasusi ya…………………………

Shule ya Sekondari **KORIDO** ipo umbali wa kilometa 25 Mashariki mwa Wilaya ya Namtumbo barabara ya kwenda Mtwara.Usafiri wa basi kutoka mjini Songea unapatikana katika kituo cha Mabasi Seed-Farm Songea – Manispaa, nauli ni shilingi 6,000/=. Aidha, Utatakiwa kuripoti Shuleni tarehe itakayo tangazwa na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI bila kukosa.

**2. Mambo muhumu ya kuzingatia:**

**2.1. Sare ya shule**

a) Shati nyeupe mbili mikono mifupi (Mashati mawili au zaidi)
b) Kwa wasichana ,Sketi mbili za rangi ya Damu ya Mzee zenye rindabox mbele na nyuma zenye urefu Sentimita 15 toka unyayoni (**SKETI FUPI HAZIKUBALIKI)**.
c) Kwa Wavulana suruali mbili (02) rangi ya Damu ya Mzee yenye marinda mawili (**NGWASUMA NA MODO HAZIKUBALIKI**).
d) Viatu vyenye rangi vyeusi vya kufunga na kambana vyenye visigino vifupi.
e) Soksi nyeupe (jozi mbili).
f) Sweta la shule rangi ya Damu ya Mzee.
g) Nguo za kushindia,(Shamba dress)
   (i). **Wasichana**: Gauni rangi ya Dark Blue,mshononi solo.Gauni liwe na urefu wa sintimeta 15 kutoka unyayoni (**GAUNI FUPI HALIKUBALIKI)**.
   (ii). **Wavulana**:Suruali rangi ya Dark Blue,yenye marinda mawili (**NGWASUMA NA MODO HAZIKUBALIKI**).
h) Hijabu ifanane na sare za shule (Nyeupe na DarkBlue).
i) Sare ya Msikitini kwa wanafunzi wa Kiislamu.
   Kwa wanafunzi wa kiume,watavaa sare ya shule,wanafunzi wa kike Vazila Msikitini litakua:
   - ✓ Suruali bluu ya heshima na isibane
   - ✓ Blauzi bluu ndefu ipitemagoti na yenye mikono mirefu.
   - ✓ Hijabu ya tetroni nyeupe/juba na sio mtandio,isiwe na urembo wowote.Pia isiwe na urembo wa lessi.

j) Sare ya michezo,traksuit nyeusi zenye michirizi myeupe pembeni.
k) Tshirt zinapatikana shuleni kwaTshs15,000/=
l) Mkanda mweusi wangozi wakuvalia suruali.

## 2.2 Michango ya shule

**a) MICHANGO MBALIMBALI**

i. Mchango wa uendeshaji wa shule 65,000/=
ii. Tahadhari 5,000/=
iii. Nembo 5,000/=
iv. Kitambulishochashule 5,000/=

**Jumla 80,000/=**

b) Akaunti No.**0150000WAYN00 CRDB (SHULE YA SEKONDARI KORIDO-EK**) na mwanafunzi afike na risiti ya kutumia fedha Benki. Tafadhali nasisitiza hatutapokea fedha mkononi..

**c) Mahitaji Mengine Muhimu kwa Mwanafunzi.**

i. Awe na sanduku (nunua sanduku la bati) linalofunga vizuri kwa kuhifadhia nguo na vitu vyake.
ii. Aje na godoro la ukubwa wafuti 2½kwa futi 6.
iii. Aje na Mtona Foronya yake
iv. Blanket moja lafuti 2½x6
v. Aje na bed cover (shuka mbili) ya blue baharifuti 2 ½ x 6 na foronya ya blue bahari visivyo na maua au urembo wowote.
vi. Shuka za Kulalia mbili za futi 2½x6 (bluebahari)
vii. Kwa wasichana,aje na Kanga au kitenge doti moja au zaidi
viii. Taulo moja (01) au mbili (02)
ix. Koti la mvua au mwavuli
x. Kandambili kwa ajili ya kuogea.
xi. Viatu vya plastiki bajaji nyeusi–vyakushindia.
xii. Aje vifaavi fuatavyo:
  a. Jembe moja(01) lenye mpini na kwanja moja (01)
  b. Squeezer kwa ajili ya kudekia/kukaushia maji sakafuni.(mopa)
  c. Ndoo ndogo mbili (moja kwamatumizi ya shule na nyingine kwa matumizi yake binafsi bwenini).
  d. Fagio la chelewa mbili (02) kwa muhula,,nne(04)kwa mwaka.
  e. Brashi ngumu yenye mpini mfupi wa mbao/mti moja (01) kwa ajili ya kusafishia sinki la choo. Asilete yenye mpini wa plastic.
  f. Alete container lenye mfuniko/sahani,bakuli,kikombe na kijiko.
  g. Daftari (counterbooks) quire three zisizo pungua kum (11) kwa ajili ya kutunzia notes.
  h. Daftari nyingine aina yoyote kwa ajili ya mazoezi kwa kila somo.

i. Aje na dictionary
j. Graph pad nne (04) kwa mwaka,
k. Ream moja ya karatasi A4 (photocopypaper) kila muhula, Rimu 2 kwa mwaka
l. Jalada/faili mbili kwa kujitunzia nyaraka zake za kitaaluma (matumizi yake binafsi) (folder files)
m. Mathematical set moja (01) kwa matumizi yake awapo darasani.
n. Alete chandarua chamsitatili, rangi nyeupe/blue cha kitanda cha futi2½ x 6.
o. AleteTsh.50,400/=kwa ajili ya bima ya afya kwa mwaka (kwa wale ambao hawana Bima ya Afya).

   Ni muhimu sana kwani itamsaidia kutibiwa kwa mwaka mzima sehemu yoyote nchini.

Fedha hii sio sehemu ya mchango wa shule, hivyo alete fedha taslimu. Asiingize kwenye akaunti ya shule.

## 3. Fedha za Matumizi

Mzazi anashauriwa akupatie fedha za kutosha kwa matumizi yako binafsi. Aidha, mwanafunzi haruhusiwi kuweka fedha Bwenini, mkabidhi Mhasibu akutunzie. Vilevile Mzazi/Mlezi atume fedha ya matumizi ya mwanafunzi kwa kupitia namba ya shule ambayo itatolewa au **0762281200/ 0715281200** (**Godlove Emanuel Chumi**) **Mkuu waShule.**

Mzazi ukitumia fedha line ya shule/ Mkuu wa Shule, aandike ujumbe kumtambulisha mhusika aliyetumiwa kwa kubainisha

i. Jina laMwanafunzi
ii. Kidato
iii. Kiasi kilichotumwa
iv. Jina la wakala au Mzazi/Mlezi aliyetuma

Aidha, Mwanafunzi hata pata ruhusa ya kwenda kufuatilia fedha sehemu nyingine. Mfano kwa ndugu nje ya shule, Benki, n.k

**NB:**Hii ni kwa fedha za matumizi tu.

## 4. Chakula

Shule hutoa chakula ambacho huliwa na Watanzania wote, ambacho Serikali inapendekeza kuliwa na mwanafunzi. Endapo unayo miiko ya kutokula vyakula fulani, tafadhali usipokee nafasi hii kwani shule haitatoa huduma ya pekee kwa kila mwanafunzi. Pia shule haitoi kibali kwa mwanafunzi kujipikia hivyo asilete chakula kama mchele, unga, biskuti, mkate, kinywaji cha aina yoyote n.k. na haturuhusu mwanafunzi kununua aina yoyote ya chakula/kinywaji toka nje ya shule

## 5. MAKOSA YATAKAYO SABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

5:1. Wizi
5:2. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
5:3. Kugoma au kuhamasisha mgomo

5:4. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake,walimu/walezi na jamii kwa ujumla.

5:5. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi,kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule.

5:6. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wa wapo shuleni. (**KUSUKA HAKURUHUSIWI**)

5:7. Kufuga ndevu

5:8. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya

5:9. Uvutaji wa sigara

5:10. Uasherati, uhusiano wa jinsia moja,kuoa au kuolewa

5:11. Kupata ujauzito au kutoa mimba

5:12. Kushiriki matendo ya uhalifu,siasa na matendo yoyote yale yanayo vunja sheria za nchi

5:13. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana

5:14. Kumiliki Kamera, Redio au kifaa chochote cha electronics isipokua Calculator

5:15. Kumiliki kipasha joto (Heater)

5:16. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni

5:17. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi kifaa chochote kinachohusiana na simu katika mazingira ya shule

5:18. Kudharau bendera ya Taifa

5:19. Kufanya jaribio lolote la kujiua,au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.

5:20. Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi

5:21. Kumiliki silaha ya aina yeyote.

## 6. Viambatanisho na Fomu Muhimu

6.1 Form ya uchunguzi wa afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospital ya serikali. Fomu hiyo ijazwe baada uchunguzi wa dakitari wa afya ya mwanafunzi. (imeambatanishwa).

6.2 Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai. (imeambatanishwa).

6.3 Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipia ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule. (imeambatanishwa).

6.4 Picha nne (04) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kutembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

6.5 Kivuli cha taarifa ya matokeo ya kidato cha nne. (resultslip) na picha nne passport size.

6.6 Kivuli cha cheti cha kuzaliwa.

## 7. ANGALIZO KWA MZAZI/MLEZI

**7.1.** Shule inafuata mihula inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi,hivyo inakuwa na mihula mirefu miwili na mifupi miwili kwa mwaka. Mzazi/mlezi unaombwa kutoa ushirikiano wako kuhakikisha mtoto anawasili kwa wakati shuleni, vinginevyo sheria itachukua mkondo wake.

**7.2.** Mawasiliano yoyote kati ya mwanafunzi na mzazi/mlezi yafanyike kupitia Mkuu wa shule, Makamu mkuu wa shule na ofisi ya Malezi .Mwanafunzi **haruhusiwi kuwa na simu ya mkononi awapo shuleni**.

**7.3.** Shule haina utaratibu wa kuwaona wanafunzi isipokuwa mzazi ataitwa na uongozi wa shule kama kuna ulazima wa kufanya hivyo.

**7.4.** Aidha unashauriwa kutomruhusu mwanao kumiliki simu kipindi hiki ambacho umri wake unampa shida kuyatawala mazingira ya utandawazi.

**7.5.** Mzazi/mlezi kutompa mtoto fedha nyingi ambazo zitamfanya apoteze utulivu wa maisha ya shule na kuvunja sheria za shule.

**7.6.** Shule ina utaratibu wa kushughulikia usafiri kwa wanafunzi wanaotoka mbali kipindi shule inapofunga. Hivyo mzazi/mlezi utapewa taarifa kabla ya shule kufunga.

**7.7.** Mzazi hakikisha unapima afya ya mwanao kwa uaminifu ili kuepuka usumbufu wakati wa masomo.

**7.8.** Iwapo mwanao ana ugonjwa unaomsumbua mara kwa mara,tafadhali aje na vyeti pamoja na dawa anazotumia na akabidhi kwa Muuguzi/Matron wa Shule.Hii itarahisisha shule kumhudumia. Usipofanya hivyo shule itashindwa kumhudumia. Usifiche ugonjwa, utapokelewa tu, kupata elimu ni haki yako.

**7.9.** Mwanafunzi anaruhusiwa kuleta pasi ya mkaa kwa ajili ya kunyooshea nguo zake. Ni marufuku mwanafunzi kuwa na kutumia pasi ya umeme ama kifaa chochote kinachotumia umeme. Akibainika hatua kali zitachukuliwa dhidi yake ikiwemo kusimamishwa shule.

**7.10.** Shule itakapokuwa imefunga, likizo zote mwanafunzi atatokea shuleni moja kwa moja kwenda kwa mzazi wake (nyumbani kwao) na shule itakapofungua atatokea nyumbani kwao (kwa mzazi) moja kwa moja kuja shuleni **akiwa na Sare ya shule**. Atakayekiuka utaratibu huu atarudishwa nyumbani kwa gharama zake.

**7.11.** Mwanafunzi haruhusiwi kuja na simu, kumiliki simu au kifaa chochote kinachohusiana na simu, hata kama anatoka mbali. **AKIJA NAVYO ATAFUKUZWA SHULE (ATAFUTWA SHULE MARA MOJA).**

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBUNI SANA KATIKA SHULE YETU**

**GODLOVE.E.CHUMI**
**MKUU WA SHULE**

*Kiambata'A'*

## TAARIFA MUHIMU ZA MWANAFUNZI.

Shule inapenda kupata taarifa muhimu za kila mwanafunzi kwa ajili ya mawasiliano Wakati wote awapo shuleni.

**Fomu hii ijazwe kwa usahihi na ukamilifu**.

Jina la Mwanafunzi…………………………………………..............……Me/Ke Kidato.........
Tahasusi ……………….. mwaka **…....**Anwani…………………….ya nyumbani (inayotumika).
Namba ya simu (ya Nyumbani/ya mzazi) ………………………………………………………
Mtaa/Kijiji anachotoka……………………………Kata…………………………..
Tarafa…………………….. Wilaya…………………………..Mkoa ………………………. Shule ya Sekondari atokayo……………………………………………………………….
AnwaniyaShule…………………………………Namba ya Mtihani ya Kidato cha Nne………… Dini yake ni …………………………………………….. (Mkristo, Mwislamun.k.)
Sahihi……………………………Tarehe……………………………

## TAARIFA YA MZAZI/MLEZI.

Jina la Mzazi/Mlezi………………………….....................………………………………………….
Anwani yake……………………………..............………Namba ya simu………………………… Kazi anayofanya……………………………….........………………………………………………
Wilaya/Mji anakofanyiakazi……………………………………………………………………………..
Anwani ya kazini………………………………….............………………………………………..
Namba ya simu ya kazini…………………………..............................………………………….

## WATU WA KARIBU NA FAMILIA AMBAO UNGEPENDA WAPATE TAARIFA ZAKO ZAIDI YA WAZAZI/WALEZI.

Jina…………………………………..................................................................................…..
Anwani……………………………………………………..Namba ya Simu………………………
Kazi anayofanya……………………..................................................................................…..
Uhusiano wake na Mwanafunzi……………………………………………………………….

Jina…………………………………..................................................................................…..
Anwani……………………………………………………..Namba ya Simu………………………
Kazi anayofanya……………………..................................................................................…..
Uhusiano wake na Mwanafunzi……………………………………………………………….

Jina…………………………………..................................................................................…..
Anwani……………………………………………………..Namba ya Simu………………………
Kazianayofanya……………………..................................................................................…..
UhusianowakenaMwanafunzi……………………………………………………………….

## AHADI.

**A: MWANAFUNZI**.

JinalaMwanafunzi……………………………………………………………………………………..
Anuani…………………………………………… Tarehe……………………………
Mimi…………………………………………………….........…………………………………………
Nimesoma maagizo ya Shule kwa makini na kuyaelewa,Naahidi kuwa mtiifu Ni tazingatia sheria.Taratibu za shule kama nitakavyo elekezwa.

**B: MZAZI/MLEZI.**

Mimi……………………………………….....…………Mzazi/Mlezi wa……………………………
Nimesoma kwa makini maagizo ya shule yaliyotolewa yanayomuhusu mtoto

Wangu.Ninakubali kuwa mwanangu achukue nafasi hiyo.Ninaahidi pia nitashirikiana na Uongozi wa shule katika kumkuza na kumlea mwanafunzi huyu **Kielimu na kitabia.**

Sahihi ya Mzazi/Mlezi................................................Tarehe............................................................

*Kiambata'B'*

UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

MINISTRY OF EDUCATION SCIENCE, TECHNOLOGY AND VOCATIONAL TRAINING

KoridoSecondarySchool
P.O.Box 55
**NAMTUMBO**

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.

**Part.A.**
**To Medical Officer**

…………………………………………………

Ref.……………………………………………………………………………………………………
(*Name in full*)

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time Schooling course at Korido Secondary School.

Your sincerely.

THE HEADMASTER KORIDO SECONDARY SCHOOL P.O. BOX 55 NAMTUMBO

**GODLOVE .E.CHUMI**
HEAD OF SCHOOL

**Part B. MEDICAL CERTIFICATE.**

(To be Completed by Government Medical Officer)
I have examined the above named student and I consider that he/she is physically fit/unfit,mentally fit/unfit for a fulltime schooling course.

I. (a)Eye-sight………………………………. (b)Hearing……………………………… (c)Limbs…………………………………… (d)Speech……………………………....

II. Neuroses…………………...........................................................................………………

III. OtherSeriousdiseases...................................................................................................................

.......................................................................................................................................................

IV. Date……………………………………… Signature…………………………………

Station……………………………………………….. Designation………………………………….

## ORODHA YA VITABU

1. **HISTORY**
   - EdwardJohn (2011), **AdvancedLearnersHistoryForm5and6**. Oxford University Press (T) LTD.
   - Shibitali & Tumaini (2011) **Recent Historical Surveys**.DaresSalaam,Shibitali & Sons Publishers. (1&2).
   - Mastering of History Book One and Two,Advanced Learners History for Form5 and 6.
   - SalehYassin,**Essentials in Advanced Level History Paper 1&2**. Ahmadiyya Printing Press.
   - Mwl.KatoA.K **Mastering AdvancedL evel History**.MweasBookPublishersand Suppliers Mwanza Tanzania.
2. **CHEMISTRY**
   - S.KSAIN (2016)**Conceptual Chemistry for Class XI and XII**,S.ChandSchool Books.
   - A.Bahl,B.S.Bahl&G.DTuli(2012) **Essential of Physical Chemistry**,S.Chand& Company Pvt. Ltd.
   - N.K. VERMA, S.K KHANNA &B. KAPILA (2012**) Comprehesive Chemistry Volume I&II for Class XII**,Laxmi Publication(P) Ltd Golden Home NewDelhi.
   - G.DTuli&R.DMADAN(2011)**Advanced Inorganic Chemistry**,S.Chand& Company Ltd.
3. **BIOLOGY**
   - Taylor (D.J), **Biological Science 3$^{rd}$ Edition**
   - Glenn Geta (1999), **New Understanding Biology For Advanced Level,4$^{th}$ Edition**, Oxford University Press.
4. **GEOGRAPHY**
   - **Physical Geography in Diagrams For Africa**(R.B.Bunnett).
   - **Practical Geography for Africa** (JohnM.Pritchard).
   - **Physical Geography**(D.T.Msabila).
   - **Human and Economic Geography**(G.C.Morgan).
   - **Geography An Integrated Approach**(DavidWaugh).
   - **Principles of Physical Geography**(F.J.Monkhouse)
   - **Atlas**
   - **Lanforms in Africa**(CollinBuckle)
   - **General Geography**(R.B.Bunnet)

5. **GENERALSTUDIES**
   - **Understanding General Studies for Advanced Level** by Joannes Bigirwamungu and Sospeter M. Deogratias.
   - **General Studies for Advanced Level Certificate Form Five and Six** by Richard R.F Mbalase.

6. **KISWAHILI**

   **(a) RIWAYA**
   - Vuta N'kuvute
   - Mfadhili
   - Usiku Utakapokwisha

**(b) TAMTHILIYA**

- Kivuli Kinaishi.
- Morani.

**(c) USHAIRI**

- Kimbunga
- ChunguTamu
- Fungate ya Uhuru

**(d) SARUFI**

- Samakisa
- Samikisa
- Kitangulizi cha Tafsiri by Mwansoko.
- Nadharia ya Lugha by Nyangwine.
- Kamusi ya Kiswahili Sanifu.

## 7. ENGLISHLANGUAGE

**(a) PLAYS**

- Betrayal In the City–FrancisImbuga
- I Will Marry When I Want–NgugiwaThong'o andNgugiwaMirii.
- Th eBride–AustineBukenya.
- Lwanda Magere–OkoitiOmtatah.
- An Enemy of The People–HenrickIbsen
- Black Mamba–John Ruganda

**(b) NOVELS**

- Encounters From Africa–Macmillan Education Limited
- The Beautiful Ones Are Not Yet Born–Ayi Kwei Armah
- A Man of The People–Chinua Achebe
- Divine Providence–everin N. Ndunguru
- The Rape of ThePearl–Magala Nyayo
- Vanishing Shadow–Namige Kayondo
- His Excellencey The Head of State–DannySato
- A Season of Waiting –David Omowale

**(c) POETRY**

- Selected Poems–Tanzania Institute of Education (TIE)
- The Wonderful Surgeon and Other Poems–CharlesMLoka

**OTHER ENGLISH LANGUAGE BOOKS**

- ADVANCED LEVEL ENGLISH, APRACTICALAPPROACH 2nd EDITION–NicholousAsheli.
- OXFORD ADVANCED LEVEL DICTIONARY 8th EDITION
- ADVANCED ENGLISH FORM 5 AND 6,1st EDITION–OXFORD UNIVERSITYPRESS, John J.
- ENGLISH PHONETICS AND PHONOLOGY–PeterRoach.
- ADVANCED LEVEL LITERATUREF ORM5 AND 6 –GodfreyRulta Bukagile.M